



Sio rahisi kuwa kama Chui Milia  
Ndio ,Chui Milia ni warembo tena wakali



Lakini Chui Milia pia ni wakubwa tena wazito.  
Hali hii inafanya iwe vigumu kwao kuwinda chakula.



Kwa kila mara ishirinii Chui Milia huwinda,  
yeye hula mara moja.




Wakati Chui Milia anapotembea porini

**KHAU! KHAU! KHAK!**

Jamii ya nyani huita, kama mtu mzee anavyokohoa!

**KHAU! KHAU! KHAK!**



**AWOOOO! HAWOOOO!**

Kubweka kwa kulungu.huita kama mbwa mwoga!

**AWOOOO! HAWOOOO!**



**OOW! OOW! OOW!**

Kulungu wa madoadoa huita kama ndege mdogo!

**OOW! OOW! OOW!**



Pori zima hujua Chui Milia yupo hapa!

**AHUUUN? AHUUN?**

Chui Milia hushangaa, wote wameenda wapi?

